Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 3, Issue 5

21st Dhul-Qa'dah 1431

29nd October, 2010

Yaliyomo

Makosa Yanayofanywa Kila... 1– 4

Advertisement 3

Makosa Yanayofanywa Kila Mara Na Mahujjaj

Mtayarishi: Sheikh 'Abdul-'Azeez Bin 'Abdullaah Bin Baaz (رحمه الله)

LA KWANZA: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA *Ihraam*

Baadhi ya Mahujjaj hukwepa vituo teule vya Ihraam wanapokuwa njiani pasi na emma kuwa na Ihraam au kuingia ndani ya *Ihraam* hapo, wakiendelea hadi wafike Jeddah au baadhi ya sehemu nyengine ndani ya vituo vilivyo chini ya masharti, ambapo ndipo wanapoingia kwenye Ihraam. Huku ni kwenda kinyume na amri ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambayo humshurutisha kila mwenye kuhijji aingie kwenye *Ihraam* kwenye kituo cha *Ihraam* kilichoko kwenye njia yake. Likimtokea mtu jambo hili, itamlazimu emma arudi kwenye kituo chake cha *Ihraam* kilichoko kwenye njia yake aliyojia na hapo ndipo aingie kwenye *Ihraam*, au itamlazimu atoe kafara kwa kuchinja kondoo akiwa Makkah na awalishe nyama yake yote watu masikini. Hilo litatekelezwa bila ya kujali iwapo mtu amepitia kwenye kituo cha Ihraam kwa njia ya angani, baharini au nchi kavu. Iwapo mtu hakupitia kwenye mojawapo ya njia tano za vituo teule vya *Ihraam*, basi ataingia kwenye *Ihraam* katika kituo kilicho karibu na kituo cha *Ihraam* kilichoko kwenye njia yake.

LA PILI: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA Twawaaf

1. Kuanza *twawaaf* kwenye sehemu isiyokuwa upande wa Jiwe Jeusi, haliyakuwa ni lazima kuanza *Twawaaf* kutoka kwenye Jiwe Jeusi.

2. Mtu kufanya *twawaaf* ndani ya *Hijr* ya Ismaa'eel, yenye maana ya kulizunguka sehemu ya *Ka'bah* badala ya kulizunguka *Ka'bah* lote, kwani *Hijr* ya Ismaa'eel ni sehemu ya *Ka'bah* ambayo baade huwachwa kando ya *twawaaf*. *Twawaaf* kama hiyo haifai.

3. Kufanya *ramal* (yaani; kutembe haraka-haraka kwa hatua fupifupi) katika mizunguko yote saba, haliyakuwa *ramal* inatakiwa kufanywa kwenye mizunguko mitatu ya kwanza peke yake ya *Twawaaf* ya kuwasili (*Twawaaf al-qudum*).

4. Kung'ang'ana kwa nguvu katika kulibusu Jiwe Jeusi, na mara kuwapiga na kuwasukuma watu. Vitendo kama hivyo, vyenye kuwajeruhi Waislamu haviruhusiwi, wala kuwapiga au kuwasukuma au kuwatusi Waislamu wenzako bila ya sababu inayostahiki.

* Watu na watanabahishwe yakwamba kutolibusu Jiwe Jeusi hakuharibu *Twawaaf* ya mtu hata chembe; *Twawaaf* itabaki kuwa ni yenye kufaa bila ya huko kulibusu. Iwapo mtu hafanyi au hawezi kulibusu Jiwe Jeusi, inatosheleza kwa urahisi aliashirie, na kusema "*Allaahu Akbar*" pindi atakapokuwepo sambamba nalo, hata kama atakuwa mbali nalo.

5. Mtu kulipangusa Jiwe Jeusi kwa mikono yake, akiona "Baraka" hapo ni jambo la uzushi (bid'ah), lisilokuwa na msingi wowote katika Sharee'ah ya Uisalmu. Sunnah ni kuligusa au kulibusu peke yake ikiwa linaweza kufanywa kwa urahisi.

6. Kuzigusa pembe nne za *Ka'bah* au kuta zake, na mtu kuzipangusa sehemu hizo kwa mikono yake. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakugusa sehemu yoyote ya *Ka'bah* isipokuwa Jiwe Jeusi na pembe ya *Yemeni*.

7. Kusoma visomo maalum vya Du'ah vilivyowekwa kwenye kila mzunguko. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakutuwekea na maombi isipokuwa kusema "*Allaahu Akbar*" kila anapolifikia Jiwe Jeusi, na mwishoni mwa kila mduara baina ya pembe ya Yemeni na Jiwe Jeusi, alikuwa akisema, "*Rabbanaa aatinaa fid-dunyaa hasanatan wa fil-Aakhirati hasanatan wa qinaa Adhaaban Naar* **("Mola wetu tupe yaliyo mema hapa Duniani na utupe mema katika Aakhira na utulinde na adhaabu ya Moto").**

8. Kupaaza sauti kuliko sauti za wengine, emma katika kufuata au kuongoza *Twawaaf* kwa vile jambo hili husababisha rabsha miongoni mwa wenye kuabudu.

9. Kung'ang'ania kuswali kwenye kituo cha *Maqaam* Ibraahim (عليه السلام). Huku ni kuikhalifu Sunnah, licha ya kuwa ni lenye kusababisha majaraha kwa wenye kuabudu. Inatosheleza kuswali *rakaa'ah* mbili za *Twawaaf* baada ya

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

Kwa Niaba ya Al-Hudaa, Tunawatakia Waislamu wote wanaokwenda Hajj, kila la kheri katika kuitekeleza Ibada hiyo Tukufu. Twamuomba Allaah , Awafanyie yaliyo na Sahali kwao, na Awatakabalie Du'ah zao. Aameen.

Makosa Yanayofanywa Kila Mara Na Mahujjaj

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

mtu kukamilisha *Twawaaf* popote ndani ya Msikiti Mtukufu.

LA TATU: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA SA'Y

1. Wanapoupanda mlima wa *Swafaa* na *Marwah*, baadhi ya mahujjaj huelekea Ka'bah na kuashiria (hali ya kulielekea) kwa mikono yao na huku wakisema "*Allaahu Akbar*" kama jinsi wanavyotamka *takbeer* wakiwa kwenye swala. Huku kuashiria ni makosa kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliinua mikono yake kwa kuomba *Du'ah* peke yake. Hapa unaweza kumuadhimisha na kumtukuza Allaah (سبحانه وتعالى), umuombe kwa matamshi yoyote upendayo haliyakuwa umeelekea Ka'bah. Imependekezwa kusoma *dhikr* ambazo alizozisoma Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa kwenye *Swafaa* na *Marwah*.

2. Mtu kuongeza kasi yake ya mwendo katika masafa yote kamili baina ya milima miwili. Sunnah ni mtu kuongeza kasi ya mwendo baina ya milingoti miwili ya kijani peke yake, na kutembea mwendo wa kawaida katika masafa ya njia yaliyobaki.

LA NNE: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA 'ARAFAAT

1. Baadhi ya mahujjaj hueka kambi nje ya mipaka ya '*Arafaat* na kubakia hapo mpaka jua likutwe; kisha huondoka kuelekea Muzadalifah bila ya kusimama '*Arafaat* kama inavyostahiki. Hili ni kosa kubwa ambalo ni lenye kuibatilisha Hajj zao kwani kisimamo chao wakiwa 'Arafaat ndicho kiini cha Hajj, na ni waajib kuwa ndani ya mipaka yake na wala sio nje yake. Ikiwa si rahisi kufanya hivyo, wanaweza kuingia kabla ya kutwa kwa jua wabakie hapo mpaka baada ya kutwa kwa jua. Ni jambo lenye kuruhusiwa kusimama '*Arafaat* katika usiku wa kuchinja hususan.

2. Kuondoka kutoka '*Arafaat* kabla ya kutwa kwa jua hairuhusiwi, kwa sababu Mtume (صلى الله عليه وسلم) alibakia '*Arafaat* mpaka jua likatwa kikamilifu.

3. Kushindana na kupigana kumbo na makundi ya watu ili kuupanda mlima wa 'Arafaat hairuhusiwi kwa sababu husababisha madhara zaidi na watu kuumizana. Uwanja wote wa '*Arafaat* ni mahali pa kusimama, na wala hakuna katika *Sharee'ah* ya Uislamu kuupanda mlima wa '*Arafaat* wala kuswali hapo.

4. Kuomba du'ah haliyakuwa umeuelekea mlima wa '*Arafaat* ni makosa kwa sababu Sunnah ni kuelekea *Qiblah* unapo-Omba du'ah.

5. Kutayarisha mirundiko ya vijiwe au ardhi: katika siku ya 'Arafaat, kwenye sehemu maalum, na baadhi ya watu, ni jambo lisilo na msingi wowote katika *Sharee'ah* ya Allaah (سبحانه وتعالى).

LA TANO: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA MUZDALIFAH

Baadhi ya mahujjaj huanza kukusanya vijiwe vya kurushwa Mina katika Nguzo za Mawe pindi tu wanapowasili *Muzadalifah* kabla ya kuswali swala ya *Maghrib* na '*Ishaa*', wakidhania yakwamba vijiwe vyote ni lazima vikusanywe *Muzadalifah*. Msimamo wa sawa ni kwamba vijiwe vinaweza kukusanywa mahali popote ndani ya mipaka ya *al-Haram* (mipaka au eneo la *Makkah*). Inajulikana yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakupendekeza kukusanyiwa vijiwe vya *jamratul-Aqabah* kutoka *Muzadalifah*. Alikusanyiwa vijiwe hivyo, asubuhi, baada ya kuondoka kutoka *Muzdalifah*, alipoingia Mina. Vilevile vijiwe vyengine akakusanyiwa kutoka Mina. Baadhi ya Mahujjaj huosha vijiwe hivyo, lakini jambo hilo halikupendekezwa.

(Endelea kwenye Ukurasa wa 4)

SHEIKH UNIFORMS

SHEIKH UNIFORMS

DEALERS IN UNIFORMS AND GENERAL SUPPLIES

- SCHOOL UNIFORMS
- SAFETY WEAR
- CORPORATE WEAR
- INDUSTRIAL UNIFORMS
- PROMOTIONAL ITEMS
- EMBROIDERY/PRINTING



ENQUIRIES:

Main Office
P.O. BOX 2192, MOI AVENUE,
KARIMI HSE, GROUND FLOOR(NEXT TO TUSKS)
TEL:041 2316749/041 2315075, MSA, KENYA
MOBILE: 0724 173362/ 0733 768250
WEBSITE: www.sheikhuniform.com
EMAIL: sheikhuniforms@yahoo.com

WORKSHOP
BAJUNI ROAD PATEL SAMAJ,
TEL: 041 2316749
MOBILE: 0727 284484

OTHER BRANCH(OPENING SOON)
MWEMBE TAYARI ROAD
OPP. GURU NANAK PRIMARY SCHOOL

Makosa Yanayofanywa Kila Mara Na Mahujjaj

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 2)

LA SITA: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA URUSHAJI WA VIJIWE

1.Baadhi ya Mahujjaj hudhania yakwamba pale wanaporusha vijiwe kwenye Nguzo za Jiwe, huwa wanawarushia Mashetwani; kwahiyo huwa wanayarusha kwa ghadhabu na nguvu. Hatahivyo, urushaji wa vijiwe ni amri tu kama njia ya kumkumbuka Allaah (سبحانه وتعالى).

2. Baadhi ya watu hurusha mawe makubwa, viatu au vipande vya mbao. Huku ni kupinduka mipaka kwenye mas'ala ya ki-dini ambako kulikokatazwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), lililoruhusiwa ni kurusha vijiwe vyenye kipimo cha tembe za haragwe.

3. Kusukumana na kupigana na wengine mukiwa kwenye Nguzo wakati wa kurusha vijiwe hairuhusiwi. Lililoamrishwa ni kuwa mpole na kurusha vijiwe bila ya kumdhuru mtu yoyote kadiri ya iwezekanavyo.

4. Kuvirusha vijiwe vyote kwa pamoja ni makosa. Wanavyuoni wamesema yakwamba hiyo itahesabiwa kama mrusho mmoja. *Sharee'ah* imeamuru kurusha vijiwe kimoja baada ya chengine, huku ukisema "*Allaahu Akbar*" katika kila mrusho mmoja.

5. Kumchagua muakilishi akurushie vijiwe, kwa kuchelea vurumai la watu au kwa kuona uzito, haliyakuwa uwezo wa kulifanya hilo unao. Mtu mgonjwa au aliye na udhaifu anaruhusiwa kuwakilishwa kwenye kitendo hicho.

LA SABA: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA *TWAWAAF* YA KUAGA (*TWAWAAF AL-WIDAA'*)

1.Siku wanapokwenda zao, baadhi ya Mahujjaj huwenda Makkah kutoka Mina kabla ya kurusha vijiwe kwenye Nguzo. Wao hufanya twawaaf yao ya kuaga, wakarudi Mina kurusha vijiwe, na wakasafiri kutoka Mina kuelekea kwenye nchi zao wanazoishi, ili nguzo yao ya mwisho ikawa ni kurusha vijiwe kwenye Nguzo badala ya kuwa ni *twawaaf* ya Ka'bah, ingawa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Mtu na asiondoke pasi na kuifanya ziyara yake ya mwisho kuwa ni kwenye Nyumba ya Ka'bah*."

Kulingana na hali ilivyo, *Twawaaf* ya kuaga ni lazima itekelezwe baada ya mtu kukamilisha nguz zote za Hajj na ikawa ni muda mchache tu wa kuanza safari ya kuelekea nyumbani. Baada ya *Twawaaf* hii mtu na asibakie tena Makkah isipokuwa kwa muda utakaomchukuwa kujitayarisha kusafiri.

2. Baada ya kumaliza *Twawaaf* ya kuaga, baadhi ya watu hutembea kinyume-nyume, huku wameielekea Ka'bah, wanapotoka nje ya Msikiti Mtukufu, wakidhania yakwamba huku ni kuiheshimu Ka'bah. Hiki ni kitendo cha Uzushi (bid'ah) katika dini na wala halina msingi wowote.

3. Baada ya kutekeleza *Twawaaf* ya kuaga, baadhi ya Mahujjaj husimama kwenye mlango wa Msikiti Mtukufu na kuanza kusoma du'ah. Huu pia ni Uzushi usiokuwa na msingi wowote katika *Sharee'ah* ya Uislamu.

LA NANE: MAKOSA YANAYOHUSIANA NA KUFANYA ZIYARA KWENYE MSIKITI WA MTUME

1. Kugusa na kuipangusa mikono kwenye kuta na nondo za vyuma, kufunga nyuzi kwenye nondo za vyuma vya dirisha, na vitendo vyengine vya sampuli hiyo wakati wa kuzuru kaburi la Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa ajili ya kupata *baraka*, yote hayo ni mambo ya uzushi (bid'ah). Baraka hupatikana kutokamana na kuyafuata ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) waliyotuamrisha, na wala sio kufanya mambo ya uzushi.

2. Kwenda kwenye mapango ya Mlima Uhud au kwenye mapango ya Mlima Hira au Thaur karibu na Makkah na kuangika vipande vya vitambara au kuomba du'ah hapo hayakuamrishwa na . Allaah (سبحانه وتعالى). Huku kote ni kujitesa kusikokuwa na maana yoyote, uzushi katika dini, na hayana msingi wowote katika *Sharee'ah* tukufu iliyotakasika.

3. Vilevile, kuzuru baadhi ya sehemu kwa kudhania yakwamba sehemu hizo zina "kumbukumbu za masalio" ya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Kama kwa mfano mahali alipowahi kukaa Ngamia wake, kisima cha 'Uthmaan au kisima cha Pete, na kukusanya mchanga kutoka hapo kwa ajili ya kupata "*baraka*", yote hayo ni mambo ya uzushi.

4. Kuwalingania waliokufa wakati wa kufanya ziyara kwenye makaburi ya Baqee au makaburi ya mashahidi wa Uhud, na kurusha mapeni kwa ajili ya kupata baraka ya mahali hapo au watu waliozikwa hapo, ni makosa ya kuhuzunisha. Kwa hakika hiyo ni Shirk (kumfanyia Allaah (سبحانه وتعالى) washirika) kama ilivyotajwa na wanavyuoni. Imedhihiri katika Kitaab cha Allaah (سبحانه وتعالى) na Sunnah za Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) yakwamba kila aina ya Ibada ni zenye kumstahiki Allaah Peke yake. Hairuhusiwi kuwalingania, au kuchinja, kula kiapo au sampuli yoyote nyengine ya Ibada isipokuwa kwa Allaah (سبحانه وتعالى) Peke yake. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى): **"Na wala hawakuamrishwa illa wamuabudu Allaah ilhali ya kumpwekesha Yeye peke yake,".** [al-Bayyinah 98:5]. Na pia akasema Allaah (سبحانه وتعالى): Twamuomba Allaah Aliye Juu zaidi azisahilishe hali za Waislamu na awape ufahamu wa dini, na atuepushe sote na makosa na upotofu. Kwa hakika, Yeye ni mwenye Kusikiya, na mwenye Kuitikiya.